

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



TAARIFA KWA UMMA

23 Machi, 2017

USALAMA WA DAWA AINA YA IBUPROFEN

1. Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ni wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto yenye jukumu la kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba.
2. Kwa lengo la kujiridhisha kuwa dawa zilizopo nchini zinakidhi usalama, ubora na ufanisi, Mamlaka imeweka mifumo mbalimbali ya udhibiti ikiwa ni pamoja na mifumo ya tathmini na usajili, ukaguzi, uchunguzi wa kimaabara, ufuatiliaji wa usalama na ubora wa dawa kwenye soko.
3. Hivi karibuni kumekuwepo na taarifa zinazosambazwa kwenye mitandao kuhusu dawa aina ya **Ibuprofen** kusababisha madhara yanayopelekea matatizo ya mshutuko wa moyo. Taarifa hiyo inatokana na utafiti uliofanyika nchini Denmark wa kuchunguza kama dawa zinazotumika kupunguza maumivu, homa na uvimbe zinazojulikana kitaalamu kama “*Non – Steroidal Anti-inflammatory Drugs*” (NSAIDs) hazisababishi madhara ya moyo. Taarifa za utafiti huo zilichukuliwa kutoka kwenye rejista ya wagonjwa waliohudhuria hospitali miaka ya 2001-2010 ambao walipata matibabu kwa kutumia dawa ya **Ibuprofen**.
4. Kufuatia taarifa hiyo, TFDA inapenda kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo:
 - (i) Dawa aina ya **Ibuprofen** inayotumika nchini kutoka viwanda mbalimbali imesajiliwa na TFDA kwa ajili ya kutuliza maumivu na kuondoa uvimbe unaosababishwa na magonjwa mbalimbali kama vile magonjwa ya viungo, mifupa, uvimbe wa fizi na maumivu ya kichwa.
 - (ii) Dawa hizo zilisajiliwa baada ya Mamlaka kujihakikishia kuwa zinakidhi vigezo vya ubora, usalama na ufanisi kutokana na taarifa zilizokuwepo wakati wa usajili. Aidha, Mamlaka huendelea kufuatilia usalama wa dawa husika baada ya usajili kwa kupokea taarifa kutoka kwa watendaji wa afya na wananchi kwa kutumia fomu maalumu za njano na kijani ambapo hakuna tatizo lolote la moyo lililotolewa taarifa TFDA kutoka katika hospitali au kwa wagonjwa.

- (iii) Tunapenda kusesitiza kwamba dawa ya **Ibuprofen**, kama ilivyo kwa dawa nyingine, ina madhara yanayofahamika ikiwa ni pamoja na kusababisha vidonda vya tumbo, kuharisha, kutapika na kuwashwa mwili. Aidha, tahadhari inatakiwa kuchukuliwa endapo mgonjwa anayetumia dawa hii atakuwa na matatizo ya moyo, shinikizo la damu au mshituko wa moyo.
- (iv) Kutokana na taarifa hii wananchi wanashauriwa kutotumia dawa hiyo kiholela bila ushauri wa kitaalamu wa Daktari na Mfamasia. Pia inasisitizwa kutotumia dawa hiyo kwa kiwango kikubwa (zaidi ya 1,200mg kwa siku) kwa muda mrefu.
- (v) TFDA inapenda kutoa tahadhari kwa wataalam wa Afya kuwafuatilia kwa karibu watu wenye matatizo ya moyo, shinikizo la damu au mshituko wa moyo na kuwapatia dawa mbadala za kutuliza maumivu ambazo ni salama ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza.
5. Aidha, Mamlaka inawahakikishia wananchi kwamba kupitia mifumo iliyopo itaendelea kufuatilia usalama wa dawa hiyo kwenye soko ili kuhakikisha kuwa dawa hiyo inaendelea kuwa salama kwa watumiaji.
6. Wito unatolewa kwa wananchi kuwa endapo watabaini au kuhisi kwamba dawa walizotumia zimesababisha madhara ya kiafya watoe taarifa TFDA kupitia mifumo ya utoaji taarifa za madhara ya dawa kwa njia ya kielektroniki www.tfda.go.tz/adr au kujaza fomu maalum na kuziwasilisha katika ofisi za Kanda zilizopo Mwanza, Arusha, Mbeya, Dodoma, Dar es Salaam, Mtwara na Tabora au kupitia ofisi za Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya.
7. Mwisho, TFDA inatoa wito kwa wananchi kuepuka kusambaza taarifa zisizohakikiwa na TFDA kupitia mitandao ya kijamii ili kuondoa hofu na taharuki zisizo za lazima.



Hiiti B. Sillo

**Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Chakula na Dawa,
S.L.P 77150,
Dar es Salaam.**